IBN KHALDUN LEARNING ACADEMY

EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# RIPOTI YA PROGRAMU YA KUIMARISHA MAADILI KWA MITAA YA WILAYA YA WETE

## MWAKA 2024/1446







ikhla.info@gmail.com www.ikhla.co.tz

IKLHA +255 773 180 921

# Yaliyomo

- Utangulizi
- Historia ya Programu
- Malengo na MisingiProgramu
- Mada Zilizoshughulikiwa
- Matokeo ya Programu
- Mafanikio na Changamoto
- Tathmini ya Programu
- Mapendekezo
- Hitimisho

IBN KHALDUN LEARNING ACADEMY
EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# UTANGULIZI

Maadili ni msingi wa maendeleo endelevu ya jamii yoyote. Wilaya ya Wete, kupitia programu ya IKHLA, inatekeleza mpango wa kuimarisha maadili, elimu ya dini, na ushiriki wa kielimu kwa watoto na vijana. Lengo kuu ni kuhakikisha kila mwanafunzi na mwanajamii anapata fursa ya kujifunza maadili bora, kuimarisha elimu ya dini, na kushiriki kikamilifu katika madrasa na skuli.

Programu hii ilihusisha mitaa minne:

- **Bubujiko**
- **Uchozini**
- **Mji Mwema**
- **Gawani**

Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, programu inalenga kutatua changamoto zinazokumba jamii na kuinua kiwango cha maendeleo ya kijamii na kiroho.




IBN KHALDUN LEARNING ACADEMY
EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# HISTORIA YA PROGRAMU

Kabla ya kuanzishwa kwa programu hii, changamoto mbalimbali ziliathiri maadili na elimu ya dini katika jamii, ikiwa ni pamoja na:

- *Uelewa mdogo wa elimu ya dini ya Kiislamu.*
- *Mahudhurio duni ya wanafunzi katika madrasa na skuli.*
- *Upungufu wa walimu wa dini na rasilimali za kufundishia.*
- *Uhamasishaji mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa maadili bora.*

Programu hii ilianzishwa ili kukabiliana na changamoto hizi kwa kupitia uhamasishaji wa jamii, utoaji wa mafunzo, na kuhakikisha watoto na vijana wanapata fursa ya kujifunza maadili bora kupitia madrasa na skuli.



# MALENGO YA PROGRAMU

1. Kuongeza mahudhurio ya madrasa kwa watoto wote wanaopaswa kuhudhuria.
2. Kuboresha mahudhurio ya skuli kwa wanafunzi katika mitaa minne: Bubujiko, Uchozini, Mji Mwema, na Gawani.
3. Kuhamasisha utekelezaji wa swala kwa wakazi wa maeneo husika.
4. Kutoa usaidizi wa kielimu na kijamii kwa watoto mayatima na wale wenye changamoto maalum.
5. Kujenga uelewa wa jamii kuhusu maadili bora kupitia uhamasishaji na kampeni maalum.

# MISINGI YA PROGRAMU

Programu hii imejengwa juu ya misingi ya Kiislamu na mafundisho ya kidini yanayohimiza malezi bora.

*"Enyi mlioamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kila nafsi iangalie yale inayoyatanguliza kwa ajili ya kesho..." Qur'an 59:18*

*Hadithi ya Mtume Muhammad (SAW) "Kila mmoja wenu ni mchungaji, na kila mmoja ataulizwa kuhusu aliyoyachunga." (Bukhari & Muslim)*

IBN KHALDUN LEARNING ACADEMY
EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# Mada Zilizoshughulikiwa

## Elimu ya Maadili na Dini

- UMUHIMU WA MAADILI KATIKA JAMII.
- ELIMU YA DINI KAMA MSINGI WA MALEZI BORA.
- KUWAHAMASISHA VIJANA KUSHIRIKI MADRASA NA IBADA.

## Elimu Rasmi na Mahudhurio ya Skuli

- KUBORESHA MAHUDHURIO YA WANAFUNZI KATIKA SKULI.
- USHIRIKIANO WA JAMII KATIKA KUHAMASISHA ELIMU RASMI.

## Ibada ya Swala na Ustawi wa Kiroho

- KUHAMASISHA UTEKELEZAJI WA SWALA KWA WANAJAMII WOTE.
- KUIMARISHA USHIRIKIANO KATI YA FAMILIA NA VIONGOZI WA DINI.

# MATOKEO

| S.N | VIPENGELE VYA MAADILI | MAJINA YA MITAA YA WANADARSA LA MAADILI | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 01 | TAARIFA ZA MADRASA | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA MADRASA | 113 | 117 | 230 | 47 | 42 | 89 | 53 | 28 | 81 | 15 | 09 | 24 | 228 | 196 | 424 | 54% | 46% | 100% |
| | WANAOHUDHURIA MADRASA | 90 | 97 | 187 | 42 | 39 | 81 | 44 | 25 | 69 | 14 | 09 | 23 | 190 | 170 | 360 | 45% | 40% | 85% |
| | WASIOHUDHURIA MADRASA | 23 | 20 | 43 | 05 | 03 | 08 | 09 | 03 | 12 | 01 | 00 | 01 | 38 | 26 | 64 | 9% | 6% | 15% |
| 02 | TAARIFA ZA SKULI | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA SKULI | 113 | 117 | 230 | 47 | 42 | 89 | 53 | 28 | 81 | 15 | 09 | 24 | 228 | 196 | 424 | 54% | 46% | 100% |
| | WANAOHUDHURIA SKULI | 104 | 115 | 219 | 45 | 41 | 86 | 46 | 26 | 72 | 14 | 09 | 23 | 209 | 191 | 400 | 49% | 45% | 94% |
| | WASIOHUDHURIA SKULI | 09 | 02 | 11 | 02 | 01 | 03 | 07 | 02 | 09 | 01 | 00 | 01 | 19 | O5 | 24 | 5% | 1% | 6% |
| 03 | TARIFA ZA IBADA YA SWALA | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA SWALA (5) | 197 | 202 | 399 | 61 | 51 | 112 | 59 | 46 | 105 | 15 | 15 | 30 | 332 | 314 | 646 | 51% | 49% | 100% |
| | WANAOSWALI SWALA (5) | 112 | 135 | 247 | 27 | 24 | 51 | 21 | 33 | 54 | 06 | 08 | 14 | 166 | 200 | 366 | 25.5% | 31.5% | 57% |
| | WASIOSWALI SWALA (5) | 85 | 67 | 152 | 34 | 27 | 61 | 38 | 13 | 51 | 09 | 07 | 16 | 166 | 114 | 280 | 25.5% | 17.5% | 43% |

# KABLA YA PROGRAMU

## Muhtasari wa Matokeo:

- Kwa madrasa, jumla ya wanafunzi wanaopaswa kuhudhuria ni 424, lakini 360 wanahudhuria, na 64 hawahudhurii.
- Kwa shule, wanafunzi wanaopaswa kuhudhuria ni 424, lakini 400 wanahudhuria, na 24 hawahudhurii.
- Kwa ibada ya swala, wanafunzi wanaotakiwa kuswali ni 646, lakini 366 wanatekeleza, huku 280 hawaswali.

## Uwiano wa Asilimia:

- 85% ya wanafunzi wanahudhuria madrasa, huku 15% hawahudhurii.
- 94% wanahudhuria shule, 6% hawahudhurii.
- 57% wanatekeleza swala zote tano, huku 43% wakikosa.

**IBN KHALDUN** LEARNING ACADEMY

EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# MATOKEO

| S.N | VIPENGELE VYA MAADILI | MAJINA YA MITAA YA WANADARSA LA MAADILI | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 01 | TAARIFA ZA MADRASA | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA MADRASA | 101 | 110 | 211 | 41 | 39 | 80 | 58 | 31 | 89 | 18 | 10 | 28 | 218 | 190 | 408 | 54% | 46% | 100% |
| | WANAOHUDHURIA MADRASA | 91 | 96 | 187 | 36 | 35 | 71 | 46 | 25 | 71 | 17 | 08 | 25 | 190 | 164 | 354 | 47% | 40% | 87% |
| | WASIOHUDHURIA MADRASA | 10 | 14 | 24 | 05 | 04 | 09 | 11 | 07 | 18 | 03 | 00 | 03 | 29 | 25 | 54 | 7% | 6% | 13% |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 02 | TAARIFA ZA SKULI | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA SKULI | 101 | 110 | 211 | 41 | 39 | 80 | 58 | 31 | 89 | 18 | 10 | 28 | 218 | 190 | 408 | 54% | 46% | 100% |
| | WANAOHUDHURIA SKULI | 99 | 106 | 205 | 40 | 36 | 76 | 55 | 29 | 84 | 17 | 10 | 27 | 211 | 181 | 392 | 52% | 44% | 96% |
| | WASIOHUDHURIA SKULI | 02 | 04 | 06 | 01 | 03 | 04 | 03 | 02 | 05 | 01 | 00 | 01 | 07 | O9 | 16 | 2% | 2% | 4% |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| 03 | TARIFA ZA IBADA YA SWALA | BUBUJIKO | | | UCHOZINI | | | MJI MWEMA | | | GAWANI | | | JUMLA KUU | | | ASILIMIA % | | |
| | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | WANAOLAZIMIKA SWALA (5) | 185 | 244 | 429 | 62 | 58 | 120 | 67 | 50 | 117 | 19 | 15 | 34 | 333 | 367 | 700 | 48% | 52% | 100% |
| | WANAOSWALI SWALA (5)4 | 138 | 155 | 293 | 30 | 32 | 62 | 41 | 41 | 82 | 11 | 08 | 19 | 220 | 236 | 456 | 31% | 34% | 65% |
| | WASIOSWALI SWALA_(5) | 47 | 89 | 136 | 32 | 26 | 58 | 26 | 09 | 35 | 08 | 07 | 15 | 113 | 131 | 244 | 16% | 19% | 35% |

# BAADA YA PROGRAMU

## Muhtasari wa Matokeo na Uwiano wa Asilimia

1.**Taarifa za Madrasa**

- Wanaolazimika kuhudhuria: 408 (kupungua kutoka 424).
- Wanaohudhuria: 354 (87%, ongezeko kutoka 85%).
- Wasiohudhuria: 54 (13%, pungufu kutoka 15%).
- Mahudhurio yamepungua kwa idadi lakini uwiano umeongezeka.

2. **Taarifa za Shule**

- Wanaolazimika kuhudhuria: 408 (kupungua kutoka 424).
- Wanaohudhuria: 392 (96%, ongezeko kutoka 94%).
- Wasiohudhuria: 16 (4%, pungufu kutoka 6%).
- Mahudhurio yameimarika kwa asilimia, na idadi ya wasiohudhuria imepungua.

3. **Taarifa za Ibada ya Swala**

- Wanaolazimika kuswali: 700 (ongezeko kutoka 646).
- Wanaoswali mara 5: 456 (65%, ongezeko kutoka 57%).
- Wasioswali mara 5: 244 (35%, pungufu kutoka 43%).
- Ongezeko kubwa la wanaoswali mara tano kwa siku, nidhamu ya ibada imeimarika.

**Hitimisho**

- Mahudhurio ya shule yameboreshwa (96%).
- Mahudhurio ya madrasa yamepungua kwa idadi lakini yameimarika kwa asilimia.
- Utekelezaji wa ibada ya swala umeongezeka kwa kiwango kikubwa.

# Mafanikio na Changamoto

## Mafanikio

- Mahudhurio ya madrasa yaliongezeka katika mitaa yote, huku Gawani ikiwa na kiwango cha juu (96%).
- Mahudhurio ya skuli yaliboreka kwa kiasi kikubwa, hasa katika Bubujiko (95%) na Uchozini (97%).
- Ushiriki wa wazazi na viongozi wa jamii uliongezeka, kusaidia kusukuma ajenda ya maadili na elimu.
- Washiriki walipata uelewa mpana wa umuhimu wa swala, huku maeneo mengi yakionyesha nia ya kuboresha utekelezaji wake.
- naopata mafunzo maalum ya kufundisha somo hili.

## Changamoto

- Viwango vya utekelezaji wa swala bado ni vya chini, haswa katika Uchozini (46%) na Gawani (47%).
- Ukosefu wa miundombinu bora ya madrasa na skuli unasababisha baadhi ya watoto kushindwa kuhudhuria masomo.
- Baadhi ya wazazi hawana uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa elimu rasmi na dini, jambo linalohitaji juhudi zaidi za uhamasishaji.
- Changamoto za kifedha kwa familia maskini zinaathiri mahudhurio ya watoto katika madrasa na skuli.

# MAPENDEKEZO



Programu ya Kuimarisha Maadili kwa Mitaa ya Wilaya ya Wete imefanikiwa katika nyanja nyingi, ingawa bado kuna maeneo yanayohitaji maboresho zaidi.

Mapendekezo

1. Kuongeza usaidizi wa kifedha na vifaa kutoka kwa serikali na wafadhili ili kuboresha miundombinu ya madrasa na skuli.
2. Kuhamasisha jamii kupitia mikutano na kampeni za maadili ili kuhakikisha kila mtoto anapata fursa ya elimu rasmi na ya dini.
3. Kutoa mafunzo maalum kwa walimu wa madrasa na skuli ili kuwawezesha kufundisha kwa mbinu za kisasa.
4. Kuhamasisha utekelezaji wa swala kwa kushirikiana na viongozi wa dini na taasisi za kidini.
5. Kuweka mfumo wa motisha kwa familia zenye changamoto kwa kuwasaidia kifedha na kimkakati ili watoto wao waendelee na masomo.

# HITIMISHO NA WITO KWA JAMII

Tunatoa mwito kwa viongozi wa serikali ya wilaya na wafadhili kuunga mkono programu hii kwa hali na mali. Mchango wenu unaweza kuwa wa kifedha, kimkakati, au kiraslimali ili kusaidia watoto na jamii kwa ujumla.

*Allah anasema: "Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika Njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipusha mashuke saba, katika kila shuke mna punje mia..." (Qur'an 2:261)*

Kwa kushirikiana, tunaweza kuimarisha maadili, kukuza elimu, na kuinua jamii kwa ujumla.

.

IBN KHALDUN LEARNING ACADEMY
EMBRACE LEARNING TO NUTURE YOUR POTENTIALS

# Wasiliana nasi

+255 776 394 494/ +255 773 180 921

iikhla.info@gmail.com

www.ikhla.co.tz

